

## **MKATABA WA KUPANGISHA NYUMBA.**

**MKATABA HUU UMEFANYIKA LEO TAREHE 1 MWEZI WA JANUARI MWAKA  
2022**

**KATI YA**

**MUHINA MOHAMED SHOMARI** wa S.L.P 109299, Arusha, Ambaye kwenye  
mkataba huu atafahamika kama **(MWENYE NYUMBA/ MPANGISHAJI)**

**NA**

**ADAM CLEMENTS SAFARIS LTD** wa S.L.P 20787, Ambaye kwenye mkataba huu  
atafahamika kama **(MPANGAJI)**

**KWAMBA**, Pande zote mbili za mkataba zimeafikiana kwa pamoja pasipo shuruti ya  
upande wowote, na kufanya makubaliano ya kupangishiana nyumba kwa makubaliano  
yafuatayo;

### **KWA KUWA;**

1. **MWENYE NYUMBA** ndiye mmiliki halali wa nyumba hiyo iliyoko maeneo ya  
Plot No. 586, Block DD, Nairobi Road, Sakina, Arusha.
2. **MWENYE NYUMBA** ana hiari ya kumpangishia **MPANGAJI** nyumba ya kuishi  
kwa makubaliano ya mkataba huu.
3. Na kuwa **MPANGAJI**, kwa hiari yake, yupo tayari kupanga chuumba hicho  
kinachopangishwa kwa kufuata, bila kuvunja masharti yanayoainishwa katika  
mkataba huu,

### **MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO;**

#### **KWA UPANDE WA MPANGAJI:**

- 1.**KWAMBA**, atatumia chumba hicho tu kwa ajili ya kuishi/ biashara.
- 2.**KWAMBA**, atalipa kodi yote kama ilivyokubaliwa na kwa muda  
uliokubaliwa bila kukosa(atalipa ndio atumie na sio atumie ndo alipe).
- 3.**KWAMBA**, ataweka nyumba/chumba katika mazingira safi na bila  
kusababisha uharibifu wowote, atawajibika kwa matengenezo ya uharibifu  
uliotokea.

**4.KWAMBA**, ataruhusiwa kufanya marekebisho kwa gharama zake kwa kumtaarifu mwenye nyumba lakini kwa makubaliano. Bila hataruhusiwa kumpangishia mtu mwingine bila idhini ya mwenye nyumba.

**5.KWAMBA**, atawajibika kulipa gharama zote za umeme na maji kila anapopata bili.

**6.KWAMBA**, endapo atasitisha mkataba huu atakabidhi nyumba/chumba iliyotajwa kwenye mkataba huu kama alivyokabidhiwa.

**7.KWAMBA**, kufanya ukarabatikama mwenye nyumba hajaridhika na hali ya nyumba kama alivyokabidhiwa.

**KWA UPANDE WA MWENYE NYUMBA:**

**1.KWAMBA**, endapo mpangaji hatavunja sharti lolote basi yeye hatambugudhi kwa namna yoyote.

**2.KWAMBA**, jukumu la kulipa kodi ya ardhi ni juu yake mwenye nyumba.

**NA MWISHO PANDE ZOTE ZIMEKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

**1.KWAMBA**, kodi ya mwezi mmoja ni shilingi za kitanzania laki tatu (300,000) kwa mwezi.

**2.KWAMBA**, mkataba huu utakuwa wa miaka mitano (5) na utasainiwa tena kama pande zote mbili zitaridhia makubaliano mapya.

**3.KWAMBA**, endapo kodi itapanda mpanga atajulishwa miezi mitatu kabla.

**4.KWAMBA**, endapo mpangaji atataka kuendelea na kupanga baada ya muda wake wa kodi yake (pango) kuisha atawajibika kutoa taarifa kwa mwenye nyumba ndani ya siku thelathini (mwezi mmoja).

**5.KWAMBA**, endapo kutakuwa na kutoelewana kati ya pande hizi mbili, mwenye nyumba anaweza atoe notisi ya mwezi mmoja kwa mwenye nyumba.

**MAKUBALIANO YA MKATABA HUU:**

Tumeyasoma na kuyaelewa na kuyakubali na pande zote tumeweka saini zetu tukiwa na akili timamu, bila kushurutishwa au kulazimishwa na mtu yeyote mbele ya mashahidi wafuatao leo tarehe 1 mwezi wa Januari mwaka wa 2022.

**KWA USHUHUDA BASI,** pande zote mbili katika mkataba huu wameweka saini zao kama ifuatavyo.

Umetiwa saini na **MUHINA SHOMARI**

Leo Tarehe 01, Januari 2022

}



.....  
**MWENYE NYUMBA**

**MBELE YA:-**

.....  


**KAMISHNA WA VIAPO/WAKILI**



Umetiwa saini na **ADAM CLEMENTS SAFARIS LTD**

Leo Tarehe 01, Januari 2022

}

**MPANGAJI**


**JINA: ADAM CLEMENT**

**CHEO: MKURUGENZI**

**SAHIHI**  .....

**JINA: ANGELO MAPUNDA**

**CHEO: MKURUGENZI**

**SAHIHI**  .....